## UTANGULIZI

Kitalu ni eneo ambalo hutumika kuotesha na kutunza miche kabla ya kupandwa shambani. Kitalu cha mizabibu kiwe kwenye eneo lenye udongo tifutifu wenye rutuba, kina kirefu na lisilotuamisha maji. Kitalu kiwe karibu na chanzo cha uhakika wa maji ili kurahisisha umwagiliaji. Sehemu ya kitalu lazima iwe imekingwa na vizuizi vya upepo. Kitalu kiwe sehemu inayofikika kirahisi na karibu na makazi ili kurahisisha uhudumiaji.

## UTAYARISHAJI WA KITALU

- Fyeka na kuchoma masalia yote ya mimea na kung'oa visiki.
- Tifua udongo kwa trekta au jembe la mkono kina kisichopungua sentimita 30.
- Changanya mbolea ya samadi na udongo kwa uwiano wa 1:8 ( toroli 1 la mbolea katika eneo la mita 8)
- Changanya mbolea yenye virutubisho vya Naitrojeni, Fosforasi na Potashi (N.P.K) yenye uwiano wa 2:1:1

## AINA ZA VITALU VYA MIZABIBU

- Kitalu cha matuta yakuinulia (Raised seed bed).
- Kitalu cha matuta yaliyozama (Sunken seed bed).
- Kitalu cha viriba / vikasha

### Uandaaji wa matuta yakuinulia

Matuta ya namna hii hufaa sana maeneo yenye mvua nyingi.

- Pima matuta yakiwa yamekinga mteremko.
- Nafasi toka tuta mpaka tuta ni sentimita 60.
- Kina cha tuta ni sentimita 20 hadi 30.
- Inashauriwa upana wa tuta uwe sentimita 60 au 90 ili iwe rahisi kuhudumia.

### Uandaaji wa matuta yakuzama

- Pima matuta kwa upana wa sentimita 60 au sentimita 90.
- Kingo za tuta ziwe sentimita 15.
- Nafasi kati ya tuta na tuta sentimita 60.

## UZALISHAJI WA MICHE BORA YA MIZABIBU

Kuna njia mbalimbali za uzalishaji wa miche ya mizabibu. Njia rahisi na inayotumika zaidi ni ya kutumia matawi.

## UCHAGUZI WA MATAWI KWA AJILI YA MICHE BORA


- Mkulima anashauriwa wakati mzuri wa kutambua matawi kwa ajili ya miche bora ni wakati mimea ikiwa na matunda.
- Matawi yawe yaliyokomaa vizuri.
- Matawi yatokane na mizabibu isiyo na mashambulizi ya wadudu na magonjwa
- Tawi liwe na unene wa milimita 9 -11 (sawa na unene wa kalamu ya risasi).
- Pingili za tawi ziwe za wastani (zisiwe karibu sana au mbalimbali sana kwani hii ni dalili ya uzaaji duni).
- Wakati wa kukata matawi, hakikisha unakata katikati ya tawi; usikate nchani wala shinani.

### Jinsi ya kuandaa makatwa (Cuttings)

Katwa ni kipande cha tawi kilichoandaliwa kwa ajili ya kupanda. Katwa liwe na sifa zifuatazo:

- Urefu wa sentimita 15 hadi 20 ili kupata macho (buds) mawili hadi matatu.
- Katwa liandaliwe kwa kuacha sentimita 1 toka jicho la chini na sentimita 4 toka jicho la juu.
- Baada ya kuandaa katwa ondoa macho ya chini libaki jicho moja la juu tu.

**Katwa la mizabibu**



## KUOTESHA MAKATWA KITALUNI

### Upandaji wa makatwa kwenye matuta

- Nafasi kati ya katwa na katwa ni sentimita 7 hadi10.
- Nafasi kati ya mstari na mstari ni sentimita 15.
- Simika katwa kwenye udongo kina cha sentimita 5 hadi 10, jicho likiwa juu ya usawa wa ardhi.
- Wakati wa kupanda tuta liwe na unyevu wa kutosha.



**Makatwa yaliyopandwa kitaluni**

### Upandaji wa makatwa kwenye viriba

- Changanya udongo, mbolea ya samadi na mchanga kwa uwiano wa 3:2:1.
- Jaza mchanganyiko huo kwenye viriba kisha panda katwa moja la mzabibu.

## UTUNZAJI WA KITALU

- Hakikisha kitalu kina unyevu wa kutosha
- Ng’olea magugu kwa kutumia  mikono
- Tifulia mara kwa mara kwa kutumia kijiti chenye ncha kali.
- Nyunyizia viuatilifu aina ya (Attakan 350, Duduba 450EC, Gammalin) kudhibiti mchwa
- Zuia wadudu waharibifu kwa kutumia viuatilifu kama Selecron na Duduba
- Dhibiti magonjwa kama ubwiri unga (Powdery mildew) kwa kutumia viuatilifu kama Xanthol na Innovex.
- Zuia magonjwa kama ubwiri vinyoya (Downy mildew) kwa kutumia viuatilifu kama Ridomil, Dithane na Mancozeb.
- **Tanbihi: Matumizi ya viuatilifu yazitangatie maelekezo ya utumiaji**

### Kuhamisha miche kwa ajili ya upandaji

- Miche ya mizabibu huwa tayari kupandwa shambani baada ya miezi minne hadi sita.
- Wakati wa kuhamisha miche kitaluni, punguza matawi na kisha acha tawi moja lenye afya na macho mawili.
- Punguza urefu wa mizizi kufikia sentimita 5-10.
- Ni muhimu kupandikiza miche mara baada ya kutoka kitaluni.

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA (TARI),
Kituo cha  Makutupora,
S.L.P 1676, Dodoma,
Simu: +255 26 2961994,
Baruapepe:cdmakutupora@tari.go.tz

**TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO TANZANIA**

TARI
Transforming Agriculture

# UTAYARISHAJI WA KITALU CHA MICHE YA ZABIBU

